

Maswali

1. Nani alisema hadithi juu ya mchungaji mwema?
2. Mbona kondoo walimfuata?
3. Mchungaji aliwapeleka kondoo wake wapi asubuhi?
4. Mchungaji mwema alifanya nini mbwa mwitu alipokuja?
5. Huyu mtu mwingine alifanya nini mbwa mwitu alipokuja?
6. Mchungaji mwema aliwapeleka kondoo wake wapi wakati wa usiku?
7. Mchungaji mwema alilala wapi?
8. Mchungaji mwema alifanya nini mwizi alipojaribu kupanda juu ya ukuta?
9. Mchungaji wetu mwema ni nani?
10. Ametufanyia nini?

Majibu

1. Yesu.
2. Kwa sababu aliwaita kwa majina yao.
3. Penye kuna kijani kibichi na maji.
4. Alifukuza mbwa mwitu.
5. Alitoroka na kondoo wengine waliuwawa.
6. Katika zizi.
7. Alilala mlangoni.
8. Alifukuza mwizi.
9. Yesu.
10. Anatujali na alitoa uhai wake kwa ajili yetu

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

36 Mchungaji Mwema

Marejeo

Johana 10: 1—15

Kiini cha somo

Kuonyesha upendo wa Yesu kama mchungaji mwema kwa kondoo wake.

Maneno maalum

1. Hadithi + mchungaji mwema + jua majina + kondoo walifuata + kijani kibichi + maji + fukuza wanyama wakali
2. Mchungaji aenda zake + mbwa mwitu + mtu atoroka + kondoo wauwawa
3. Usiku + zizi + ukuta mrefu + mchungaji nyumbani + kondoo salama
4. Mwizi + panda ukuta + mchungaji aamka + fukuza.
5. Mchungaji mwema + kondoo salama + Yesu mchungaji wetu + anatupenda + anatulinda.


36.1 Hii ni habari nyingine ambayo Yesu alisema inayohusu Mchungaji. Palikuwa na Mchungaji mwema aliyekuwa na kundi kubwa la Kondoo akiwatunza. Wote walimjua na kumpenda na yeye aliwajua wote kwa majina. Walimfuata kokote alikokwenda. Kama mchungaji mgeni angekuja na kuwaita ili wamfuata, wengemkimbia, lakini kama mchungaji wao angekuja, wote wengemkimbilia na kumfuata popote ambako angekwenda.



Asubuhi huwatangulia kondoo wake mahali penye malisho mazuri, na kwa kawaida huwapeleka penye mito yenye maji mazuri na ya baridi. Huwalinda mchana kutwa akiwalinda wasishambuliwe na wanyama mwitu. Wakati mwingine mnyama mwitu angekuja kuwaiba wanakondoo, lakini hata hivyo asingeweza kupata hata mmoja maana mchungaji mwema alikuwa mwangalifu sana wakati wote na kama angekuja mchungaji angemfukuza au kumwua.

36.2 Na endapo mchungaji angetaka kusafiri angemweka mtu mwingine kuwalinda kondoo wake. Wakati mchungaji mwema aliposafiri, mbwa mwitu alikuja na yule aliyeachiwa kondoo badala ya kumfukuza mbwa mwitu, yeye alikimbia kwa sababu aliogopa na kujali zaidi maisha yake kuliko uhai wa kondoo. Mbwa mwitu akawararua baadhi ya kondoo na waliobaki wakatimbia. Haikuwa salama kwa kondoo kuwa porini peke yao usiku. Maana mbwa mwitu wengi walikuwa wakizunguka zunguka usiku eneo lile. Jua lilipoanza kuzama mchungaji huwaiata kondoo na kuwapeleka nyumbani hadi kwenye zizi la kondoo.

36.3 Zizi hili lilizungushiwa ukuta mrefu kwenda juu, uliojengwa kwa mawe na juu yake paliwekwa miiba ili kuzuia wezi. Kulikuwa na mlango penye ukuta ambapo mchungaji mwema angepitisha kondoo wake akiwa hesabu wakati wanapoingia. Ndipo wanakondoo hulala chini ya mama zao kwa amani. Mchungaji mwema hulala nje ya mlango akiwalinda kama kuta tokea hatari.



36.4 Wakati mwingine kama mwizi angekuja kuiba baadhi ya kondoo. Asingeweza kujaribu kupitia mlango kwa sababu mchungaji angemwona na hata kama angejaribu kupanda ukuta pole pole. Hata hivyo kondoo wangemtambua kuwa huyu ni mtu mbaya na kwa sababu hiyo kondoo wangemkimbilia mchungaji wao.

36.5 Kwa hiyo mchana na usiku, kondoo walikuwa salama kwa kuwa na mchungaji wao mwema. Yesu akawambia Wanafunzi wake kuwa yeye ni mchungaji mwema na wao na sisi ndiyo kondoo wake.

Yeye anatupenda na anatumia kwa majina yetu. Anatulinda siku zote, aliutoa uhai wake kwa yetu. ni Furaha kubwa iliyoje kuwa na mchungaji mwema na mwenye upendo mkuu namna hii.

